# MWONGOZO WA KUSAHIHISHA

## KIDATO CHA 3

## KARATASI YA 2

**Ufahamu**

1. Wanakijiji walitatizwa na wanyama pori na kuwasilisha malalamiko yao kwa serikali (alama 2)
2. Ukosefu wa usalama - Mauaji
- Kuzikuliwa kwa wafu -Kutopata fidia inayostahili
- Gharama kubwa ya matibabu - Uharibifu wa mimea, makazi na nyua

(zozote 4x ½\)

3. –Kuuawa kwa mifugo
- Kudidimia kwa malisho ya mifugo
- Mifugo kuambukizwa maradhi (alama 2)

4. – Kuunda jopo la kushughulikia fidia na suluhisho
- Kuanzisha kikosi maalumu cha askari wa kulinda watu na wanyama
- Kujenga ua la umeme
- Kujenga mabwawa mbugani
- Kuimarisha idara ya tiba kwa mifugo wilayani

(4x1 = alama 4)

5. –Kuonyesha uchungu waliokuwa nao
- Kumtaka mkuu wa wilaya aone uzito wa tatizo lao

(1x1= alama 1)

6. a). Kuchukua hatua/ kutembea kwa miguu
   b). Kutekeleza jambo badala ya kungojea serikali kulitatua
   (1 x2 =alama 2)
7. i). Mateso/ taabu/ dhiki
   ii). Usumbufu/ maudhi
   iii). Wakimeza
   iv). Paneli/ kundi la watu wa kushughulikia jambo Fulani
   (1 x 4= alama 4)

**UFUPISHO**

a). – Damu kuganda katika miguu na moyo

-Kusababisha matatizo wakati wa ujauzito

-Ugumu/ shida wakati wa kujifungua

- Huathiri watoto na kuwafanya wavute sigara wakiwa wadogo

-Kifo kabla, wakati ama baada ya kujifungua

- Huathiri ubongo wa mtoto

- Huathiri ulimi wa mtoto na kumfanya mzito wa kuongea

- Huathiri mapafu ya mtoto

Hoja 6x1= alama 6

Mtiririko alama 1

Jumla alama 7

b). –Magonjwa kama kifua kikuu, kansa ya mapafu/ utumbo

- Husababisha kifo

- Moshi wa sigara husababisha uvimbe katika utumbo na rektamu

- Huleta magonjwa ya kifua k.v kikohozi, pumu, homa ya mapafu

- Husababisha magonjwa ya moyo

- Hukakamaza kuta za mishipa ya damu

- Husababisha shinikizo la damu

**MATUMIZI YA LUGHA**

a) b, d, j,g ( 2x1 = alama 2)

b) A- Nafsi

Ta- Wakati

M- Kitendewa/ mtendewa

Tawadh- Mzizi

Ish- Kauli

a- Kiishio

( kila kiainisho sahihi ½ x6 = alama 3)

c). Kucheka – kitenzi-jina

Bwana Omari – pekee

Raha – dhahania

Asali – kawaida

(1x 4= alama 4)

d). i). LI-YA

ii). I-ZI

(Atunge sentensi sahihi kudhihirisha maana) (2x 2= alama 4)

e). <u>Ufumaji</u> wake wa mikeka huwa na <u>mvuto</u> kwa wengi (1 x2= alama 2)

f). Nilimkuta Mkuu wa wilaya ya Munyaka akisoma kitabu kiitwacho “KIU”

( ½ x 4 = alama 2)

g). “Mtakuwa mkija kwetu siku zote kuniona,” Njeri aliwaambia rafiki zake.

( 6 x 1/3 = alama 2)

h). Alikuwa – Ts ( Kitenzi kisaidizi)

Akienda – T (Kitenzi kikuu) (1 x2= alama 2)

i). Kuzidisha machungu/ kudhuru zaidi

- Giza totoro (1 x2= alama 2)

j). i). Kwa dhati – kielezi namna

ii). Mno – kielezi halisi (1 x2= alama 2)

k). Udogo-

Kipaka/kijipaka kiki hiki hula kipanya/kijipanya na kunywa kiziwa kila siku

Wingi

Vipaka/ vijipaka vivi hivi hula vipanya/ vijipanya na kunywa viziwa kila siku

(2x2 =alama 4)

l). Ukimwona mwalimu usimwambie nitamtembelea kesho

Ukimwona- alama ½

Usimwambie – alama 1

Nitamtembelea-alama ½

m). Mjomba huhifadhi/ hutunza mshahara wake kila mwezi.

n). i). Mabaharia wenyewe hawangeweza kusafiri na kuwasili hiyo Ijumaa.

ii). Mabaharia wanaripoti kuwa watu wengine waliwaarifu (mabaharia) hawatawasili Ijumaa hiyo. (2 x1=alama 2)

o). Bohari- Stoo

Soko- marikiti au gulio

p) Changu kimepotea

Kioo changu kilivunjika

(Matumizi mengine sahihi ya –angu) 1x2=alama 2

**ISIMU JAMII**

a). Sajili ya lugha ya mtaani (1x2= alama 2)

b). Ni wana hirimu. Wanatumia lugha ya mtaani au sheng' ambayo hutumika sana baina ya vijana.

c). i) Ni lugha legevu isiyozingatia kanuni za kisarufi

ii). Kuna kuchanganya ndimi

iii). Hutumia misimu kwa wingi

iv). Hukosa mada maalum

v). Lugha huwa si wazi kwa sababu wazungumzaji wanaweza kukosa kumaliza kauli

vi). Kuna maswali na majibizano

(1 x6 =alama 6)

( Mwanafunzi atoe mifano sahihi kwa kila hoja)